USAWIRI WA MWANAMKE KATIKA NGANO ZA KINYANKOLE WILAYANI MBARARA KATIKA KAUNTI YA KASHARI KATIKA VIJIJI VYA KATEETE, RUHUNGA NA RWANTSINGA.

NA

NUWAMANYA JUDITH

BAE/46293/151/ DU

TASNIFU YA UTAFITI ILIYOWASILISHWA KWENYE IDARA YA LUGHA NA MAWASILIANO KATIKA KITOVU CHA SANAA NA ELIMUKUKIDHI BAADHIYA MAHITAJI YA KUHITIMU SHAHADA YA SANAA NA ELIMU YA CHUO KIKUU CHA MATAIFA KAMPALA.

APRILI 2018

UNGAMO

ndekezo hili la utafiti ni kazi yangu binafsi na haija chapishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote tika chuo kikuu chochote.

ıa:.....NUKIAMAHYA JUDITH.....

hihi:.....[signature].....

ırehe:.....19/04/2018.....

IDHINI

Tasnifu hii ya utafiti imewasilishwa kwa azima ya kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada ya sanaa na elimu katika chuo kikuu cha mataifa Kampala nchini Uganda, kwa idhiniyangu kama msimamizi niliyeteuliwa rasmi na chuo hicho

Jina la msimamizi: Atukunda Edwine

Sahihi: .....

Tarehe: 19/02/2018

TABARUKU

nifu hii ninaitabarukia wazazi wangu walionizaa; Bwana Noel Emmanuel na Bi Kenyonga drine.Pia si wezi kutoitabarukia wazazi wangu wengine walionisaidia katika masomo yangu .ka chuo; Cpt.Amanya Onesmus Kakuba na mkewe Bi Orikiriiza Vaster,marafikiwangu wa ibuBi Tusasiirwe Jonnah na Bwana Nabaasa Rodgers, mwalimu wangu Bwana Atukunda vine kwa usimamizi wake na mwongozo wake kwangu.

SHUKURANI

Namshukuru Mungu muumba wangu kwa maisha niliyonayo pamoja na afya njema aliyonipa katika kipindi nilichokuwa nafanya utafiti wangu na shughuli zote za kukamilisha utafiti wangu huu.

Pia namshukuru Bwana Atukunda Edwine, mhadhiri katika idara ya fasihi kwakunisimamia na kunisaidia vilevile. Umekuwa mzazi kwangu mungu akubariki sana.

Ningependa pia kuwashukuru wahadhira wengine katika idara ya lugha wakiwemo;Bi Mutenyo Aidah, Bwana Onyeit Wilison, na Bi Azabo Immaculate.

Siwezikutoshukuru wazazi wangu Bwana Noel Emmanuel na Bi Kenyonga Medrine kwa kunizaa , kunilea kunikuza,kunitunza,kunilipia karo kuanzia katika msingi wa masomo yangu paka hapa nilipo .Pia siwezikutoshukuru Cpt.Amanya Onesmus na mkewe Bi Orikiriiza Vaster kwa sababu wamekuwa wazazi kwangu katika masomo yangu katika chuo karo mlizonilipia umekuwa msaada mkubwa kwangu kwani mumenilea na kunipenda kama mwanao sina budi kuwaita wazazi wangu kwani matendo yao nakujitoa kwao kumenisaidia katika mambo mengi kwangu.

Pia nashukuru dadangu Tusasiirwe Jonnah, kwani umenifanyia mengi maishani mwangu asingelikuwa wewe sijui nigelikuwaje.

Pia siwezikutoshukuru dada na kaka wangu;Muhangi Micheal,Nasasiira Kevin,Ninsiima Mackline, Ainembabazi Patricia na Amutuhaire Immaculate kwa sababu ya misaada yao na,mapenzi

Pia nashukuru rafiki zangu kama Bwana Nabaasa Rodgers,Bwana Adonia na familia yake,Bi Gwokyalya Edith,Bi Betty Kamya, Bi Taligoola Deborah, Bwana Serestine na familia yake Muhairwe Ambrose na wengine wengi siwezi kuwataja hapa wote.

IKISIRI

Utafiti huu ulihusu ngano za Wanyankore wanaoishiWilayani Mbarara katika kaunti ya Kasharimagharibu Uganda.Utafiti huu uliangazia usawiri wa mwanamke kama inavyobainika katika ngano za Wanyankore waliyo katika wilaya ya Mbarara kaunti ya Kashari. Utafiti huu ulilenga kuchunguza usawiri wa mwanamke na ujumbe unaopatikana katika ngano za jamii ya Wanyankore wanaoishi katika wilaya ya Mbarara kaunti ya Kashari katika vijiji vya Kateete, Rwantsinga na Ruhunga. Tasnifu hii ilikusanya ngano kutoka katika robo za Bahima wanaoishi Rwantsinga na Bairu wa Kateete na Ruhunga. Mbinu tatu zitatumika katika hatua ya ukusanyaji wa data. Mbinu ya mahojiano, mbinu ya umakinifu na mbinu ya Udurusi wa nyaraka maktabani. Jumla ya ngano kumi zilikusanywa. Ngano zote kumi ziliteuriwa ili zilinisaidia kutafuta majibu ya utafiti huu. Utafiti ulipata majibu kwamba, ngano katika jamii hii humsawiri mwanamke katika hali mchanganyiko, chanya na hasi. Kwa hiyo, utafiti wangu ulipata majibu kwamba, zipo ngano zenye mtazamo hasi kuhusu mwanamke. Malengo ya utafiti huu yalikuwa; kuchumguza jinsi mwanamke amesawiriwa katika ngano za kinyankore, kuchanganua nafsi na majukumu ya mwanamke anavyotazamiwa katika ngano za kinyankore na kujadili haki za mwanamke katika ngano za kinyankore. Kwa hivyo ngano zilikusanywa ili kufatuta mwanamke amesawiriwa kivipi na kwa kiwango gani.Ujumbe uliopatikana katika ngano ni kwamba, mwanamke anapaswa kuthaminiwa sawa na mwanaume.

ABSTRACT.

This research focused on the folktales of Banyankore who live in Mbarara district, Kashari county in the vilages of Kateete, Ruhunga na Rwantsinga in Western Uganda. Foltales are important in the Banyankore culture about portraying vividly the image of feministy in Mbarara District.The main objective of this research will be explicity to portray divisionism of gender responsibilities and in particular the roles which empower women in social set up forexample, politically, in marriage,and economically. At least ten foltales will be sourced from twenty three old people who will be sampled from the Banyankore community in the vilages of Kateete, Ruhunga and Rwantsinga . The folktales were analyzed in order to determine how a woman is under looked in the society. .Field research method will be used to collect data and twenty people were sampled for interview were expound on the meanings and use of folktales among the Banyankore culture. And all ten folktales were taken up so as to get answers for questions.Thereafter, each individual folktale were scrutinized and analysed as per itsroles and image portrayed then a generalized conclusion shall be made over feministy in them.The findings of this research shed more light and knowledge about the image portrayed by a woman and they led way to other researchers who may wish to do further research on ~~feministy.~~ feminism

TABLE OF CONTENT

UNGAMO i
IDHINI ii
TABARUKU iii
SHUKURANI i
IKISIRI ii
ABSTRACT iii
SURA YA KWANZA 1
1.0 UTANGULIZI 1
1.2 Usuli wa utafiti 1
1.3 Swala la utafiti 2
1.4 Madhumuni ya utafiti 3
1.5 Malengo mahsusi ya utafiti ni; 3
1.6 Umhimu wa utafiti 3
1.7 Nadharia tete 3
1.8 Upeo wa utafiti 4
1.8.0 Upeo wa kijografia 4
1.8.1 Upeo wa kiufundi 4
1.8.2 Upeo wa wakati 4
1.8.3 Eneo la kitaalimu 4
1.9 Maswali ya utafiti 4
1.9.1 Shida zilizomkumba mtafiti 5
SURA YA PILI 6
MAPITIO YA MAANDISHI 6
2.0 Utangulizi 6
2.1.3 Usawiri 7
2.2 Hadhi ya mwanamke katika ngano 7
2.3 Majukumu ya mwanamke kama inavyojitokeza katika ngano. 8
SURA YA TATU 10
MBINU YA UTAFITI 10
3.0 Utangulizi 10

3.1 Njia zilizotumika katika ukusanyaji wa data 10
3.2 Njia ya mahojiano 11
3.3 Njia ya umakinifu 12
3.4 Udurusu wa nyaraka maktabani 12
3.5 Sampuli ya watu katika ukusanyanji wa data 12
3.5.1 Zana za utafiti 13
3.5.2 Kalamu na karatasi 13
3.5.3 Simu ya mkononi 13
3.5.4 Kirimbo 13
3.5.5 Ngamizi 14
3.6 Uchanganuzi wa data 14
3.6.1 Vyanzo vya data 14
3.6.2 Data za msingi 14
3.6.3 Data za upili 14
3.7 Uteuzi wa walengwa 15
3.8 Njia za kupitia walengwa 15
3.9 Uteuzi wa sampuli 15
Jedwali Na.3.2: uteuzi wa mahojiano 16
Hitimisho 17
SURA YA NNE 18
UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI 18
4.0 Utangulizi 18
4.1 Uwasilishaji wa data 18
4.3 Usawiri wa mwanamke katika ngano za jamii ya Wanyankore. 19
4.4 Tathimini ya hojaji na mahojiano 19
Jedwali 4:1 jinsia ya wahojiwa 19
Jedwali 4:2 umri wa wahojiwa 20
Jedwali 4:3 je kwa namna gani ngano za Wanyankore kumsawiri mwanamke kwa mtazamo hasi katika wilaya ya Mbarara? 20
Jedwali 4:4 ujumbe unaopatikana katika ngano za Wanyankore kuhusu usawiri wa mwanamke wilayani Mbarara. 21
Jedwali 4:5 mtazamo hasi wa mwanamke katika ngano za kinyankore 21

Jedwari 4:6 je majina, nyimbo, vitendawili na methali humsawiri mwanamke kivipi katika jamii ya wanyankore? 22
4.5 Unukuzi na tafsiri za ngano 23
4.5.1 mvumilivu 23
4.5.2 Mvumilivu kwa mume we 23
4.5.3 Mlezi wa watoto 23
4.5.4 Mwanamke hafichi siri 24
4.5.5 Mtafutaji wa chakula 24
4.5.6 Mwanamke anasawiriwa kuwa si mtu mwenye roho nzuri kwa watoto asiyewazaa 25
4.5.7 Utengenezaji vikapu 25
4.5.8 Kusaga mtama 25
4.5.9 Mwanamke nikiumbe mwenye roho mgumu katika jamii 25
4.6 Usawiri chanya wa mwanamke katika ngano za Kinyankole 25
Hitimisho 26
SURA YA TANO 27
MUHTASARI, MATOKEO YA UTAFITI NA MAPENDEKEZO 27
5.0 Utangulizi 27
5.1 Muhtasari wa matokeo ya utafiti huu 27
5.1.1 Usawiri chanya wa mwanamke 29
5.2 Usawiri wa mtazamo hasi wa mwanamke 29
5.3 Ujumbe katika ngano za jamii ya Wanyankore. 29
5.4 Mambo mapya katika utafiti huu 29
5.5 Mapendekezo 30
5.5.1 Mapendekezo kwa wanazuoni 30
5.5.2 Mapendekezo kwa wanajamii 30
5.5.3 Mapendekezokwa Serikali 30
MAREJELEO. 31
VIAMBATANISHO 33
A. Mwongozo wa hojaji 33
B. Mwongozo wa mahojiano 35
C. NGANO 36
PICHA ZILIZONASWA WAKATI WA KUKUSANYA DATA UWANJANI 63

LIST OF TABLES

Jedwali Na.3.2: uteuzi wa mahojiano 16

Jedwali 4:1 jinsia ya wahojiwa 19

Jedwali 4:2 umri wa wahojiwa 20

Jedwali 4:3 je kwa namna gani ngano za Wanyankore kumsawiri mwanamke kwa mtazamo hasi katika wilaya ya Mbarara? 20

Jedwari 4:6 je majina, nyimbo, vitendawili na methali humsawiri mwanamke kivipi katika jamii ya wanyankore? 22

Jedwali 4:5 mtazamo hasi wa mwanamke katika ngano za kinyankore 21

Jedwali 4:4 ujumbe unaopatikana katika ngano za Wanyankore kuhusu usawiri wa mwanamke wilayani Mbarara. 21

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Wanyankoreni miongoni mwa wabantu nchini Uganda. Wanyankore wanaishi katika lokeshoni nyingi za Uganda. Utafiti ulikuwa unaangalia katika Wanyankore wa Wilaya ya Mbararar kaunti ya Kashari katika vijiji vya Kateete,Ruhunga na Rwantsinga. Mbarara inapatikana kati ya latitudo 8° hadi 12° Kusini mwa Ikweta longitudo 12.3^{o} na 33.2^{o} Mashariki mwa Greenwich.Inapakana na Wilaya hizi;Bushenyi, Kiruhura,Buhweju,Ibanda,Isingiro na Lyantonde.

Wenyeji wa wilaya ya Mbarara ni Wanyankore, lakini kuna jamii za wahamiaji kama vile Banyarwanda kutoka Rwanda, Batutsi kutoka Rakai na Bakyiga kutoka Rukyiga na wengine wengi. Ardhi ya Unyihani ni nyekundu lakini yenye rutuba inayostawisha mazao, yakiwamo ya chakula k.v mahindi, maharagwe, ndizi, karanga na biashara ,uchungajiwa ngombe hasa kahawa.

Jamii ya Wanyankore ni miongoni mwa jamii za kale hapa nchini Uganda, ambayo ina historia ya muda mrefu, tangu kipindi cha maisha ya zamani hadi sasa, kwa msingi huo, jamii ina mambo mengi mema ambayo ni vema yakakusanywa na kuhifadhiwa, kwamanufaa ya wanajamii katika vizazi vingi vijavyo. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na tanzu za fasihi simulizi zilizosheheni vijitanzu kadha wa kadha zikiwemo ngano.

Utafiti huu ulikusudiwa kuchunguza usawiri wamwanamke katika ngano za jamii ya Wanyankore waishio wilaya ya Mbarara kaunti ya Kashari katika vijiji mahususi yaani Kateete, Ruhunga na Rwantsinga.

1.2 Usuli wa utafiti

Wanyakore ni miongoni mwa wabantu wanaopatikana katika viwango vingi vya Uganda. Lakini utafiti huu uliangalia katika Wanyankore wa wilaya ya Mbarara kaunti ya Kashari katika vijiji vya Kateete, Ruhunga na Rwantsinga nchin Uganda. Mbarara inapakana na Bushenyi,Rwanpara, Isingiro ,Ibanda Buhweju na Kirihura.kwa kusudi la Ngano ni utungo wenye visa vya kubuni unaosimuliwa kwa lugha nathari kuburudisha, kukuza maadili na kuunganisha jamii. Msimulizi

wa hadithi huitwa fanani au mtambaji.

Finnegan (1970) anaeleza kwamba ngano huwakilisha falsafa ya watu ambayo huwasilishwa kwa njia ya masimulizi yanayodhihilishwa kwa hisia na taswira zilizotiwa chuku. Kwa hivyo zimebeba falsafa ya Wanyankore. Utafiti huu utachunguza jinsi falsafa ya Wanyankore kuhusu usawiri wa mwanamke katika jamii ya wanyankore katika ngano.

Yunusu (2010) katika utafiti wake unahusu usawiri wa mwanamke katika methali za kinyankore, anaeleza majukumu ya mwanamke katika jamii ya wanyankore ambayo ni; kupika, kuzaa, na kadhalika. Utafiti wake ni tofauti na huu kwa kuwa yeye aliangazia usawiri wa mwanamke wa kinyamkore katika methali na utafiti huu umechunguza jinsi ngano zinavyomsawiri mwanamke katika jamii ya wanyankore.

Kulingana na kamsi ya TUKI(2004), inafafanua ngano kama hadithi fupi ambazo wazee husimulia watoto hufikiriwa na jamii kuwa kweli na hutumiwa kuwasilisha ujumbe wenye maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa. Kwa hivyo utafiti huu utachunguza jinsi ngano hizi zinavyomsawiri mwanamke katika jamii ya Wanyankore wa Wilaya ya Mbarara.

Halliday (1978), anatoa kauli kwamba mtoto anapojifunza lugha huwa anajijengea picha ya uhalisia unaomzunguka ngano kama chombo cha ufundishaji katika jamii kinachotumia lugha kama msimbowa kupitisha ujumbe wake, huakisi hali halisi ya wanajamii kwa njia hii.

Mazrui na siambo (1992) wanaeleza kuwa ngano zinaweza kubainisha falsafa za watu Fulani kuhusu maisha yao, na huweza kuonyesha majukumu yanayotekelezwa na wanaume kwa wanawake na mieleko ya jamii husika Kulingana na wataalamu hao, ngano huwasilisha falsfa za watu kutegemea tajiriba zao za kimaisha.

Kutokana na mtazamo huo, ni muhimu kwamba uchunguzi ufanywe kwa jamii ya Wanyankore ili kubainisha hadhi ya mwanamke kulingana na jinsi alivyosawiriwa katika ngano.

1.3 Swala la utafiti

Ngano za Wanyankore zina ujumbe muhimu sana kwa vile hufunza jamii kuhusu usawiri wa mwanamke. Ujumbe ulipitishwa kwenye ngano za wanyankore ili kuonyesha njinsi Mwanamke

amesawiriwa katika jamii ya Wanyankore wilayani Mbarara. Licha ya umuhimu waujumbe unao patikana kwenye ngano, hakuna utafiti uliofanywa ili kuonyesha jinsi mwanamke amesawiriwa kivipi kupitia ngano. Utafiti huu umefanywa ili kuziba mwanya huu na kuonyesha jinsi mwanamke amesawiriwa katika ngano za Kinyankore.

1.4 Madhumuni ya utafiti

Lengo kuu la jumla la utafiti huu ni kuchanganua jinsi mwanamke amesawiriwa katika ngano za Kinyankore.

1.5 Malengo mahsusi ya utafiti ni;

a.Kuonyesha jinsi mwanamke amesawiriwa katika ngano za kinyankore.

b.Kuchanganua nafsi na majukumu ya mwanamke kwa mtazamo wa ngano za kinyankore.

c.Kuonyesha haki za mwanamke katika jamii ya Wanyankore.

1.6 Umhimu wa utafiti

Ngano zilizokusanywa zikitunzwa vizuri wengi watapata fursa ya kuzisoma na kuzizamia mbizi,kuzifanyia utafiti zaidi na kuzitumia maarifa yaliyomo. Kwa kutumia utafiti huu,wanaharakati wataatmbua namna jamii ya Wanyankore inavyomtazama mwanamke tangu jadi mpaka sasa, kwani ngano ni sanaa kongwe. Utafiti huu umetoa picha mpya juu ya usawiri wa mwanamke katika fasihi simulizi, watakaosoma utafiti huu watatambua kwamba, mwanamke anamchango mkubwa katika jamii zetu. Utafitu huu utatumika kama kitambulisho cha Wanyankore katika jamii kubwa ya Uganda.

1.7 Nadharia tete

a. Mwanamke katika jamii ya Wanyankore amesawiriwa kutokana na majukumu yanayodhihirishwa katika ngano

b Kuna uhusiano kati ya jinsi mwanamke anavyosawiriwa katika ngano za kinyankore na majukumu anayotekeleza katika jamii.

c.Mwanamke katika jamii ya Wanyankore humuweka katika ngazi ya chini katika majukumu kama yanayodhihirishwa katika ngano.

1.8 Upeo wa utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza usawiri wa mwanamke katika ngano za kinyankore waishio wilayani Mbarara nchini Uganda. Jumla ya ngano tisa (9)zilitazamiwa kuchunguzwa. Ngano zilizochunguzwa zilizingatia kubainisha jinsi fani hii inavyotumiwa kuelimisha,utamaduni na desturi za jamii, ngano zilichunguzwa kwa minajili ya kubainisha picha halisi ya mwanamke dhidi ya ile ya mwanaume; hasa kwa kuainisha jinsi mgao wa mamlaka unavyojitokeza katika jamii ya Wanyankore.

1.8.0 Upeo wa kijografia

Utafiti huu umefanyiwa katika jamii ya Wanyankore wilayani Mbarara kauntI ya Kashari-Rubaya katika vijiji vitatu yaani;Kateete, Ruhunga na Rwantsinga maghariu Uganda. Eneo hilo liliteuliwa kwa sababu idadi kubwa ya wakaazi wake wa asili ni Wanyankore, ambao ndio walengwa wa kazi hii.

1.8.1 Upeo wa kiufundi

Upeo huu ulilenga kuchunguza mbinu jinsi mwanamke amesawiriwa katikta ngano za kinyankore wilayani Mbarara katika vijiji yaani; Kateete, Ruhungana Rwanstinga ili kutafuta marekebisho mwafaka katika hali hii yakimaisha.

1.8.2 Upeo wa wakati

Utafiti ulifanywa kwa muda wa miezi mine yaani kuanzia mwezi wa Desemba hadi mwanzoni mwa mwezi wa April. Muda huu ulimsaidia mtafiti kukusanya data iliyohusu mada ya utafiti wake.

1.8.3 Eneo la kitaalimu

Katika utafiti huu, uchunguzi ulijikita katika kijitanzu cha ngano peke yake.

Usawiri wa mwanamke katika ngano za Kinyankore umeshughulikiwa pia uchunguzi ulifanyika kuhusu ujumbe unaojitokeza katika ngano za Kinyankore zile zenye usawiri wa mwanamke.

1.9 Maswali ya utafiti

i Kwa namna gani, ngano za kinyankore huwasawiri wanawake kwa mtazamo hasi katika jamii ya Mbarara.?

iiNi ujumbe gani unaopatikana katika ngano za Kinyankore.?

1.9.1 Shida zilizomkumba mtafiti

(i)Mtafiti alikumbwa na shida ya hela za kuendesha uchunguzi wake. Hata hivyo ilimbidi mtafiti kupanga bajeti yake kwa ajili ya kulenga mambo muhimu tu.

(ii) Isitoshe mtafiti alikumbana na shida ya kutoaminiwa na wahojiwa, yaani kuchukuliwa kama mpelelezi jambo ambalo lilizuia baadhi ya wahojiwa kumpokea vilivyo.

(iii)Hali kadhalika mtafiti alikumbwa na shida yakutokuwa na muda wa kutosha ili kuzingatia kazi yake vikamilifu.

(iv)Mtafiti alipata shida ya uchapishaji maana huchukua muda mwingi pamoja na hela nyingi.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI

2.0 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti atazingatia maandishi ya wasomi mbalimbli pamoja na tafiti zilizofanywa kuhusiana na mada hii. Mtafiti atamulika kwa makini machapishoyanyohusu picha ya mwanamke katika ngano za jamii ya Wanyankore.

Ni muhimu kutalii kazi zao ili kuongeza ujuzi,ubora na maarifa katika kazi yetu.Kumar (2011) anasisitiza kwamba, ipo haja kubwa ya kutalii kazi za wanazuoni waliotangulia,kwa sababu ya kupatikana nafasi ya kutambua vipengele vilivyochunguzwa na ambavyo baado.Kwa kufanya hivyo, ni rahisi kupata mapengo ya utafiti ambayo yanapaswa kuzibwa kitaalumu.

2.1 Ufafanuzi wa dhanna kama zilivyotumika katika kazi hii.

2.1.1 Jinsia

Jinsia ni kipimo kinachotumika kupima hadhi ya mtu katika jamii. Ni tofauti na jinsi,ambayomni isitilahi ya kibailojia zaidi. Jinsia inahusu mtazamo wa jamii, wanadamu wanavyopeana wajibukulingana na tofauti zao za kijinsi. Mfano wanawake wamekuwa wakipewa hadhi duni na wanajamii ikilinganishwa na wanaume,wengi wao wanaendelea kuamini kuwa, mwanamke hawezi kujitegemea mwenyewe bila mwanaume. Jambo hilo linapewa nguvu zaidi na Ripoti yaumoja wa kimataifa(1980) inabainisha kuwa, wanawake idadi yao ni kubwa zaidi kuliko wanaume, hufanya kazi zaidi ya theluthi mbili ya kazi zote. Kutokana na kazi wanazozifanyamapato yao ni asilimia kumi ya mapato yote,wanawake humiliki asilimia moja ya mali zoteduniani. Kwa kawaida tamaduni za kiafirika hufanya upendeleokwa wanaume dhidi yawanawake. Wanaume ndiyo wenye haki ya kupewa urithi wa mashamba, nyumba, ardhi na hatakushika nafasi za juu katika uongozi(women Affairs and children(1995)

2.1.2 Ngano

Ngano katika lugha ya kinyankore huitwa *ebigano* ni aina ya mafumbo yanayohitaji muda

mrefu,mafumbo hayo huwa na mianzo na miisho maalumu.kwa kusudi la Ngano ni utungo wenye visa vya kubuni unaosimuliwa kwa lugha nathari kuburudisha, kukuza maadili na kuunganisha jamii. Msimulizi wa hadithi huitwa fanani au mtambaji.

2.1.3 Usawiri

Usawiri ni istilahi katika taalimu ya kifasihi, yenye maana ya taswira za wahusika wa fasihi zinazoundwa na wasanii ili kuwasilisha tabiya ya na matendo mbalimbali ya binadamu katikamaisha halisi. Istilahi hiyo imekuwa ikitumiwa zaidi na wahakiki wanapochambua kazi za fasihi hasa katika kipengele cha wahusika. Katika mazingira hayo, wahakiki huonesha mitazamona fikra zao kulingana na jinsi walivyozielewa kazi za wasanii. Kwa hiyo usawiri ni taswira sahihi na halisi wanazostahili kupewa wahusika katika kazi za fasihi.

2.2 Hadhi ya mwanamke katika ngano

Tafiti nyingi zimefanywa kuhusu mambo ya uana ambapo mitazamo mingiimejitokeza kubainisha picha ya mrwanamke mbele ya mwanaume.Wakihoji kwa mtazamo wa udenguzi,Kennedy na Dan (2000),walisema upo ugumumkuu mwanaume kukubali kwamba yupo mwanamke mzuri duniani. wao humwona mwanamke kama mtu mwizi asiye na huruma kwa mwanaume. Mtafiti akitumia mtazamo huu, atapenda kuchunguza kama kweli picha kama hiyo yaweza kujitokezakatika jamii ya Wanynkore.

Kulingana na Kerre (1989),alifanya utafiti juu ya ndoa na utawala katika jamii zakiafrika ulimwongoza kudai kwamba itikadi na tamaduni za kiafrika haumpimwanamke uwezo wakutambuliwa kama kiongozi na mlinzi wa jamiiKwa hivyo, utafiti huu utapambanua kwa undani jinsi mwanamke anavyodhihirishakipawa cha uongozi na kwa nini alikabidhiwa mamlaka hayo.Kulingana na Harrow(1991),akitafiti kuhusu mtazamo wa dini ya kiislamu kuhusu ndoa, alisema kwamba mwanaume ndiye husheheni madarakani ya juu katika jamiisi mwanamke. Yeye alihoji ya kwamba mwanaume ni wa kuheshimiwa kila marana mwanamke si mwanaume kumheshimu mwanamke. Mtafiti akitumia mtazamohuu ,atapenda kuchunguza kama ni ukweli ama ni uongo katika ngano zakinyankore.Matteru(1991),akitafiti juu ya ngano za kinyankorekama chombo cha mawasilianokatika jamii. Alidai kwamba sina uwezo wa kuinbua mielekeo maalum yawatkulingana na utamaduni wao.Akizingatia nadharia ya kiisimu jamii

alisema kwamba tabia za mtu hudhihirikakulingana na imani ya utamaduni wake. Kwa mtazamo huo huo, utafitihuuunatazmiwa kujikita katika kutumia ndharia ya ufeministi ya kike ili kutathminimajukumu aliyonayo mwanamke wa jamii ya Wanyankore.Sunkan(1973) na Lavera (2003),wakifanya utafiti juu ya utamaduniwa Bahima naBairu walidai kwamba jamiin humlazimisha mwanamke kama chombo chanyumbani. Huyu alisema kwamba mwanamke kazi yake ni kupika na kuzaa watoto.Kwa mtazamo wa Lubeleje (1990:2),ngano zina ukweli kwa watu woteulimwenguni na mafunzo yake hayana mipaka kwa jamii yoyote ile,kwa vilehuhifadhi utamaduni na desturi za jamii husika. kama kweli ngano zina mafunzoyoyote muhimu kwa jamii ya Wanyankore utafiti huu utalenga kuthibitisha haliuchanganuzi utakaoweka wazi mitazamo na mielekeo ya hiyo kupitia kwa jamiinzima.

Bukenya na Nandwa (2000), wanasema kwamba ngan huchukuliwa kuwa kazi ya ubunifu wa watu wanaozisimulia ilihali visasili na visakale huchukuliwa kuwamatukio ya kweli. Ngano huonyesha asilimia kubwa ya wanajamii wanachoamini. Hili lilimuongoza mtafiti katika utafiti yaani lilisaidia kujumlisha kuwa ngano huonyesha kile kinachoaminima na asilimia kubwa wanajamii. Kwa hivyo yaleyanayojitokeza katika ngano yalichukiliwa kuwa yanaaaminiwa na asilimia kubwaya Wanyankore. Hili litathibitisha kuwa kinchojitokeza katika ngano kinawakilishaimani asilimia kubwa ya wanyankore kuhusu ngano kama zinazoonyesha usawiri wamwanamke. Magel (1991) ,kulingana na huyu yeye alisema kwamb, mwanaume yeye kazi yake ni kula na kujenga nyumba. Kwa maana mwanamke ndiye aliyekuwaanatarajiwa kufanya kazi zote zingine katika nyubani. Kwa sababu ya maoni hayo mwanamkeanaonekana kama anasawiriwa. Ngano nyingi za kinyankore zinzungumza juu ya hiimamboKulingana na Mwachofi yeye alisema kwamba mwanamka jamii nyingi za kiafrika ni za kuumei na humweka katika ngazi ya chini akilinganishwa na mwanamume.Ili kuinua hahi za wanawake magharibu Ugandana yameweka mikakati ya kuboreshahadhi ya mwanamke.

2.3 Majukumu ya mwanamke kama inavyojitokeza katika ngano.

Akivaga na Odaga (1982) wanashikilia kwamba ngano hudhihilisha mitazamo ya watu kuhusu maisha ya watu na huchota jazanda zake kutokana na mazingira maalum. Kwa mtazamo huo huo, Anuka (1978) aliziona ngano kama zao la utamaduni ambalo linatokana na mazingira maalum ya kijamii na picha kamili yamielekeo ya maisha hujitokeza muno humo. Kwa mjibu wa mtazamo wa Akivaga na Anuka utafiti huu ulipata nafasi ya kuchunguza jinsi majukumu ya

kijinsia yanavyojitokeza katika ngano za Wanyankore.Jennifer (1994:3), alifanya utafiti na kugundua kwamba wanaume wameanza kusaidia wanawake kufanya kazi za nyumbani. Balisdya(1987:7),anaeleza kwamba ngano ni misemo itumiwayo kuelezea kitu kwa njia ya picha na kwa ufupi ili itoe maadili Fulani.

Alisema kwamba ngano hubuniwa kwa kushikamanishwa na utamaduni, desturi na hadhi ya jamii kulingana na mazingira na makusudi ya kurahisisha hali tofauti zilizo katika jamii. Kama kigezo cha kuonyesha picha ya jambo Fulani linalokusudiwa,mtazamo wa Balisdya kuhusu ngano umempa mtafiti changamoto ya kuchunguzajinsi majukumu ya mwanamke yanavyojitokeza katika ngano za Kinyankore.

Kipuri (1983), akitafiti juu ya visasili, na visasili ni aina ya ngano inayoeleza asili auchimbuko la jamii au mambo ya kiada kama mauti, ndoa, tahara nakadharika.Visasili katika jamii ya Wanyankore vinatuonyesha jinsi mwanamke amesawiriwa.Kwa hivyo mtafiti alichunguza jinsi majukumu ya mwanamke yalivyojitokeza katika visasili vya Kinyankore Kitsao (1980),Mwachofi(1987),na Arege,(2007), waliweza kubaini jinsi fasihi kama kipengele cha utamaduni inavyobadilika. Utafiti uliongozwa kuhusu utetezi wa haki za mwanamke katika jamii ya Wanyankore. Mwanamke katika jamii ya Wanyankore anatambua kwamba amedhulumiwa na kunyimwa haki.Kwa hivyo mtafiti anapaswa kuzingatia au kubainisha na kulinganisha jinsiwahusika wa kike na kiume walivyojengwa na kutafuta kiasi cha usawiri wa mwanamke . Kulingana na Mwachofi yeye alisema kwamba mwanamka, jamii nyingi za kiafrika ni za kuumei na humweka katika ngazi ya chini akilinganishwa na mwanamume.Ili kuinua haki za wanawake magharibu Ugandana yameweka mikakati ya kuboresha hadhi ya mwanamke utafiti huu ulilenga kubainisha ni kwa kiasi gani mahitaji ya wanawake waWanyankore yanavyopambanuliwa katika ngano.

SURA YA TATU

MBINU YA UTAFITI

3.0 Utangulizi

Mbinu na njia za utafiti ni dhana zinazofanya kazi kwa pamoja katika utafiti. Deusi (2011) anazitofautisha dhana hizo kwa kuwa, mbinu ni namna au jinsi ya mtu, anavyowezakufanikisha jambo lake. Mbinu ya utafiti ni namna inayomwongoza mtafiti kuchunguzo lake hadiakalipatia suluhu. Njia ni mpito wa kuimarishia mbinu. Bailey (1994) anasema kwamba, mbinu za utafiti ni hatua za kifalsafa za mtafiti,ambazo huzitumia katika kazi yake ya utafiti, na hasa namna atakavyokusanya data,kuzichambua na kuziandikia taarifa ya utafiti kuhusu usawiri wa mwanamke katika ngano.

Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa, mbinu za utafiti, ni jumla ya taratibu zote zinazotakiwa kufuatwa katika kazi ya utafiti, njia ni mikakati anayotumia mtafiti ili kufanikisha lengo lake. Mbinu za utafiti zipo nyingi, ni pamoja na usaili, umakinifu, maswali na majibu,mahojiano nakusoma machapisho. Sevenye na Robinson(2001), wanasema, njia za utafiti,humsaidia mtafiti akubalike katika jamii na kupewa taarifa bila hofu. Katika utafiti huu, data iliyotumika ilitukana na taarifa na majibu ya maswali kadhaa yaliyoulizwa kwa watoa uwanjani.

Kimsingi, data muhimu iliyo kusanywa ni ngano zinazohusiana na usawiri wa mwanamke. Katika sura hii, mtafiti alitaja na kueleza mbinu mwafaka zilizotumiwa katika kuendeleza utafiti huo.

3.1 Njia zilizotumika katika ukusanyaji wa data

Utafiti huu ni utafiti wa uchanganuzi matini iliyoshughulikiwa ni ngano za kinyankore. Mtafiti alikusanya data ambazo ni ngano kutoka kwenye vitabu mbalimbali mkiwemo kitabu cha karwemera (1978) na asili zingine. Mtafiti alichanganua na kutathimini ngano kwa mjibu wa jinsi zinavyopitisha usawiri wa mwanamke katika jamii ya Wanyankore.Utafiti huu utatekelezwa nyanjani. Mtafiti aliwasaili ana kwa ana wazee watakaoteuliwa kumwongoza katika kupata

ngano hamsini atakazatafuta kwao,zikihusu jinsia ,na zaidi zile zinazoangazia picha ya mwanamke.Atazirekodi ngano zote zitakazotolewa katika daftari lake dogo ambamo maelezo juuya maana na matumizi ya ngano hizo yataandikwa.Haitazamiwi kutumia hojaji kwa wingi, ispokuwa tu kwa wale wazee watakaokuwana shughuli zisizowaruhusu kushiriki kikao cha uso kwa uso. Mathalan ,lokesheni zote tata zilifikiwa na mtafiti mwenyewe binafsi; na pale ambapo patakuwa na uwezekano wa kuwakusanya pamoja wasawiliwa wote patafaa zaidi kwa kuwa hiyo itasaidia mno kwa upande wa gharama ya usafiri namuda wa kuwafikia .

Ndani mwa kila lokesheni mtatazamiwa kuwa na wasaidizi wawili wawiliwalioniongoza katika kuwapata wazee watatu kwa kila lokesheni tatu.Ili kupunguza gharama ya usafiri,mtafiti atahitaji kutumia pikipiki kwa kuwa ipo nauwezo wa kufika sehemu zote za wilaya kwa uharisi. Kuhusu mamboyafundishwayo jandoni data ilipatikana kwa kuwauliza maswali wazee wanao ongoza mafunzo hayo huku nikiyarekodi katika daftari langu dogo.Pia utafiti huu ni utafiti wa uchanganuzi matini iliyoshughulikiwa ni ngano za kinyankore. Mtafiti alikusanya data ambazo ni ngano kutoka kwenye vitabu mbalimbali mkiwemo kitabu cha karwemera (1978) na asili zingine. Mtafiti alichanganua na kutathimini ngano kwa mjibu wa jinsi zinavyopitisha usawiri wa mwanamke katika jamii ya wanyankore.

3.2 Njia ya mahojiano

Hii ni njia ya kupata data kwa kutumia maswali na majibu yanayotokana na mazungumzo kati ya mtafiti na watafitiwa Kothari(2008). Kombo na Tromp(2006) wanasema kuwa katika njia hiyo,mtafiti lazima awe na mada maalumu itakayoongoza mahojiano hayo. Wanapendekeza, kuwa katika njia hiyo,kirmbo kitumike kwa ajili ya kurekodi mambo mamba yote yatakayojadiliwa.

Kwa msingi huo, mtafiti aliweza kufanya mahojiano na kundi la watu lililoandaliwa kwa kuzingatia vigezo vya waswali ya mahojiano hayo. Manufaa ya njia hii ni kwamba, humsaidia mtafiti kupata mawazo, na mwelekeo.

Baadhi ya maswali yaliyoulizwa ni; jee, ngano za jamii ya Wanyankore zinamsawiri vipi mwanamke?, Ngano hizo zinawasilisha ujumbe gani kwa jamii?

3.3 Njia ya umakinifu

Ni njia ambayo humwezesha mtafiti kuwamo ndani ya mazingira halisi ya uptikanaji wa data zinazohitajika. Leary (2001) anapendekeza kuwa, njia ya umakinifu ni nzuri zaidi kwani humfanya mtafiti kupata data katika mazingira halisi ya watafitiwa kwa kujionea mwenyeweukweli wa jambo kama inavyoonekana katika udhatiwake. Ingawa Kahn (2011)anasisitizakwamba njia hii inafaa zaidi kutumika katika mambo ya kisayansi, lakini kwa Afrika, sayansi ili pewa kazi pana zaidi kuliko sayansi ya kingereza, ambayo kimsingi ni kemia, Biolojia na Fizikia.Njia hii ni mwafaka,tumeichagua kwa sababu,inayeweka wazi mazingira ya usimliaji wa ngano.

3.4 Udurusu wa nyaraka maktabani

Udurusu wa nyaraka maktabani ni mbinu inayopendekezwa na Leary (2001) na Kumar(2010), wanasema kwamba zipo data ambazo huweza kupatika katika nyaraka zilizotunzwa maktabani na kwenye mitindo ya kielektroniki. Data hizo zinaweza kutumika katika kazi ya utafiti,jambo la msingi ni kwamba lazima pawepo na uhusiano wa mada. Katika utafiti huu baadhi ya data zilikusanywa kwa njia ya kusoma na kuchambua maandiko mbalimbali yanayohusiana na ngano. Ukusanyaji wa data hizo ulifanyika katika chuo kikuu cha Kampala International University. Mbinu ya kudurusu maktabani humsaidia mtafiti kupata maelezoya ziada yanayoshadidia data za msingi ilikuwezesha kujibu maswali ya utafiti huu.

3.5 Sampuli ya watu katika ukusanyanji wa data

Sampuli ya watu katika kazi ya utafiti ni kundi la watu wazee ambao ni wenyeji katika maenao ya utafiti,ambao huongozana na mtafiti wa ukusanyaji wa data za utafiti. Mgogo (2012) anasema,tunalazimika kuomba sampuli ya watu ambao ni wenyeji wa eneo la kiutafiti ili kupunguzaugeni wa mtafiti. Kazi kubwa ya kundi hilo ni kumtambulisha mtafiti kwa watafitiwa,kuwashawisha watafitiwa wawe na ushirikiano na mtafiti,kupunguza hofu kwa watafitiwa kuhusu mtafiti kuelekeza watu wenye kuhifadhi data zinazotafutwa katika utafiti

huutulishirikiana na uongozi wa vijiji kupata sampuli ya watu watatu katika kila kijiji tulichokusanya data hizi. Tuliambatana nao wakati wa kukusanya data. Kwa kuwa ngano ni sehemu kubwa njemaya utamaduni wa jamii, tuliomba kamati za utamaduni za michezo vijijini, zikishirikiana nawenyeviti wa vitongoji ili kupata sampuli ya watu wenye sifa. Katika utafiti huu, tulipatawazawa namaeneo husika wenye uzoefu na kuwatambua watu wenye kuhifadhi data zinazotafutwa,kwaniwao wanajuana kwa sifa, mielekeo na tabia.

3.5.1 Zana za utafiti

Zana za utafiti ni jumla ya vitu vyote ambavyo mtafiti alivitumia katika kazi ya ukusanyaji wa data. Miongoni mwa vifaa hivyo ni kalamu na karatasi,simu ya mkononi kirimbo ngamizi na kamera.

3.5.2 Kalamu na karatasi

Kalamu na karatasi ni nyenzo za kuandikiya na kuhifadhiya maandishi. Kothari (2004),anasemakwamba kalamu ni zana za msingi katika utafiti wowote wa kitaalimu. Vifaa hivyo vilitusaidia kunukuu na kuhifadhi baadhi ya kumbukumbu muhimu, kama vile majina ya wataafitiwa, tareheya kukutana baadhi ya taarifa za mahojiano yetu na walengwa.

3.5.3 Simu ya mkononi

Hiki ni kifaa cha mawasiliano kati ya mtafiti na watafitiwa. Tulikitumia kifaa hicho kufanyamakubaliano ya muda na mahali pa kukutania ili kuweza kufanya mahojiano. Katika mazingirahayo,simu ya mkononi,ilirahisisha zoezi la kukusanya data, kwani mambo mengi ya makubaliano maalumu, kati ya pande mbili, yaani mtafiti na watafitiwa.

3.5.4 Kirimbo

Kirimbo ni kifaa kinachotumika kunasia sauti za watafitiwa masikanini. Tulikitumia kifaa hicho tulipokuwa tunakusanya data kwa njia ya mahojiano na uchunguzi wa data makini. Taarifazilizorekodiwa katika kirimbo,tulizitumia katika hatua ya uchambuzi wa data.

3.5.5 Ngamizi

Ni kifaa kwa ajili ya kucharazia maandishi. Tulikitumia kifaa hicho katika mambo mawili; kwanza,kukusanyia data za upili katika wavupepe baada ya kunganishwa katika mtandao, pilitulikitumia wakati wa kuchapa ripoti ya tasnifu hii, ili iweze kusomeka katika maandishi.

3.6 Uchanganuzi wa data

Ngano zote zilikazokusanywa zilichanganuliwa kwa njia ya kimaelezo kulingana namadhumuni ya utafiti.Maelezo hayo yalihusu kubainisha jinsi ngano zinavyomsawiri mwanamke kamainavyojitokeza katika ngano za Wanyankore. Uchunguzi ulihusisha ukaguzi wangano moja baada ya nyingine kwa njia ya kuziainisha kulingana na majukumu yake.Hatimaye, muhtasari ulitolewa kwa kubainisha zile ngano zinazomsawiri mwanamke kwa picha ya uongozi ,utawala,udalimu, unyanyasaji uchumi,ubibi n.k

3.6.1 Vyanzo vya data

Data zilizotumika ndani ya kazi hii ni za aina mbili; data zilizopatikana kutokana na mkusanyiko wa majibu ya moja watafitiwa, ambazo huitwa data za msingi. Pili, data zilizopatikana kutokana na kutalii kazi tangulizi, ambazo huitwa data za upili, hupatikana katikavitabu, tasnifu, majarida,magazeti n.k

3.6.2 Data za msingi

Hizi ni data ambazo zilipatikana kutoka kwa watafitiwa baada ya kuulizwa maswali au kujadiliana na mtafiti juu ya mada ya utafiti huu. Kothari (2003) anasema,mtafiti huzikusanya mwenyewe kutoka masikanini. Masikanini ndiko wanakoishi watu.kusiko watu k.v uwandani hakufanyika utafiti wa kijamii. Katika utafiti huu, data zilizowasilishwa zilipatikana katika vijiji vya Kateete, Ruhunga na Rwantsinga.

3.6.3 Data za upili

Hizi ni data ambazo zilipatikana katika machapisho vikiwemo; vitabu, majarida, tasnifu,

magazetina matini zenye uhusiano na kazi hii. Kazi hiyo ilifanywa na mtafiti ili kujiongezea maarifa na ujuzi wa kukamilisha utafiti huu. Mwali hufundwa na wajuzi watanguzi, watu wazima, wenye tajiriba za uhalisiya wa maisha.

3.7 Uteuzi wa walengwa

Walengwa ni kundi dogo linalowakilisha kundi kubwa katika kazi ya utafiti. Creswell namwenzake (2009), Kumar (2013),Kombo na Tromp (2006) wanaeleza kwamba, walengwa ni kundi wakili la watafitiwa, linaweza kutoa majibu ya maswali ya mtafiti. Webster (1985) anasema, kundi la walengwa ni kundi la watu wachache, lililoteuliwa kutoka katika kundi la watu wengi, kwa ajili ya kufanyiwa utafiti. Katika kazi za utafiti, walengwa hupatikana katika makundi tofauti tofauti kama vile wanakijiji, wanafunzi, walimu,n.k. Cohen na Lawrence(2000) na Bryman(2004) wanasisitiza kuwa, kiwango cha ukubwa wa walengwa ,huamliwa na mtafiti mwenyewe kutokana na sababu alizonazo. Miongoni mwa sababu hizo,ni aina ya utafiti, madainayohusika, kiasi cha raslimali alizonazo mtafiti,raslimali zinazohusishwa ni muda, fedh za vifaa vya kuendesha utafiti. Katika utafiti huu, walengwa ni watu waliohifadhi ngano za jamii ya Wanyankore.

3.8 Njia za kupitia walengwa

Katika kazi ya utafiti,zipo njia zinazopendekezwa na wataalamu ili zitumike kupata walengwaTromp na Kombo(2006) wanapendekeza njia mbili. Njia ya kubahatisha ambayo mtu yeyote huingizwa katika kundi bila kutumia kigezo chochote. Njia ya matabaka, mtu huingizwa katika sampuli kulingana na vigezo vitakavyowekwa na mtafiti. Wanasisitiza kuwa, njia ya matabaka hutumika katika utafiti wa mambo ya kale, au katika mada nyeti kama utoaji wa mimba, umalaya, magonjwa,na watoto wa mitaani. Mada kama hizi zisipotafutiwa kundi maalumu lawatafitiwa, ni rahisi sana, kwa mtafiti kushindwa kupata data halisi.

3.9 Uteuzi wa sampuli

Mbinu ya uteuzi makusudi itatumiwa katika kutafuta data kuhusu ngano juu ya jinsia. Mbinu hii iliongozwa na malengo maalum ya utafiti ambayo kiini hasa ni kuchunguza jinsi ngano za Wanyankore zinavyomsawiri mwanamke kupitia kwa majukumu aliyopewa.Ngano zinazohusu ujumbe juu ya hadhi ya mwanamke zilikusanywa kutoka kwa wazee wenye umri wa miaka

hamsini na tano na zaidi walio na uelewa mwingi wa lugha ya kinyankore yaani; wane kutoka kwa kila lokesheni tatu za wilaya hiyo yaMbarara magharibu. Wazee hao walitegemewa katika utafiti huu kwa kuwa umriwao wa zaidi ya miaka hamsini na tano huwapa fursa ya kutoa ushauri na kauli maalmu katika miktadha mbali mbali ya kijamii hasa matangani, arusini, tohara na sherehe za kifahari kama za mavuno na hafla za kisasa. Jumla ya methali kumii na tarajiwa kukusanywa ili zichanganuliwe kulingana na majukumu na mielekeo yake hasa kuhusu uana.

Jedwali Na.3.2: uteuzi wa mahojiano

Kijiji	Wanawake	Wanaume	Jumla
Kateete	2	2	4
Ruhunga	2	2	4
Rwantsinga	2	2	4
Wazee wengine	4	4	8
Jumla	**10**	**10**	**20**

Chanzo ni mtafiti (2017)

Njia za uchambuzi wa data

Kipengele cha uchambuzi wa data kinahitaji umakini, utulivu na ufahamu mkubwa. Katika hatuahii, mtafiti anasauriwa kuzingatia mambo muhimu. Kombo na Tromp (2006), wanasema, kwanza ni lazima mtafiti azijue data zisizohitajika na aziondoe katika uhambuzi wake. Kothari (2003) anasema, katika utafiti wa kiulimbe, baada ya kukusaya data, mtafiti anapaswa kuzichambua data hizo kulingana na matarajio ya utafiti huo. Uhambuzi humsaidia mtafiti kupata ukweli wa madhumuni aliyojiwekea.

Taasis ya Elimu Uganda (2003) wanasema data, hutoa jibu la swali la utafiti na ili matokeo ya utafiti ya weza kuaminika lazima kukubalika lazima yachambuliwe vizuri. Data za utafiti huwa nyingi na mara kadhaa huwa katika mchanganyiko mkubwa. Mtafiti hulazimika kuzichambua kwa umakini ili aweze kutoa taarifa kamili kwa wasomaji wa kazi hiyo, kulingana na lengo lakazi yake. .

Best na Kahn (1987), wanapendekeza njia zinazofaa kutumika katika uchambuzi wa data nazo ni; kutumia asilimia endapo kuna idadi kubwa ya watafitiwa, kuchambua data kwa kutumia

wastani, hutumika ili kuelewa watu wanasema nini juu ya jambo Fulani, uchambuzi wa data kwakigezo cha uwiano, hutumika ili kupata kiasi cha uhusiano wa ongezeko au upungufu wa kipengele kimoja dhidi ya kingine.

Hata hivyo, katika utafiti huu tumetumia njia ya kimaelezo ambayo inapendezwa kutumika katika utafiti wa mambo ya sayansi ya kijamii Kothari (2008). Mkabala wa kimaelezo umetumika kwa sababu utafiti huu, hauhitaji data za uwiano na asilimia bali umejikita katika kutafuta maelezo ya kina, ukweli na uthibitisho.

Hitimisho

Sura hii imeeleza kwa kina njia au mbinu zilizotumiwa na mtafiti wakati wa ukusanyaji wa data za utafiti huu. Baadhi ya njia hizo ni mahojiano pia kuna maelezo ya matumizi ya vifaa vilivyotusaidia katika upatikanaji na uhifadhi wa data zetu, miongoni mwa zana hizo ni, kirimbo, kalamu na karatasi baada ya kukamilisha sura tatu yenye mbinu za kukusanya data, tunaingia sura ya nne yenye vipengele vya uwasilishaji na uchambuzi wa data.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI

4.0 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti amehudhurisha majibu ya maswali yaliyopatikana katika mahojiano pamoja na taarifa alizozipata katika majadiliano na uchunguzi makinifu, uliofanyika.

4.1 Uwasilishaji wa data

Uwasilishaji na uchambuzi wa data ni hatua muhimu katika kazi yoyote ya utafiti, katika hatuahii mtafiti amewasilisha taarifa zilizokusanywa na kuzifanyia upembuzi makini kwa kuzingatia malengo yaliyokusudiwa katika utafiti huu. Lengo kuu la utafiti ni kukusanya ngano, kuziainisha,kuzichunguza kwa undani na kuonesha namna zinavyowasawiri wahusika wanawake. Madhumuni maalumu ya utafiti yalikuwa;

(a) .Kujadili jinsi mwanamke amesawiriwa katika ngano za kinyankore.

(b).Kuchanganua nafasi na majukumu ya mwanamke kwa mtazamo wa ngano za kinyankore.

(c).Kujadili haki za mwanamke katika jamii ya Banyankore. Ili kufikia lengo la utafiti huu, maswali mawili yaliulizwa;

i Kwa namna gani, ngano za kinyankore huwasawiri wanawake kwa mtazamo hasi katika jamii ya Mbarara.?

iiNi ujumbe gani unaopatikana katika ngano za Kinyankore.?

Kabla ya kufikia hatua ya uwasilishaji wa data, hatua zifutazo zilizingatiwa. Kwanza, mtafiti ilirekodi ngano kwa kutumia kirimbo,vikiwa katika lugha ya Kinyankore, hatua ya pili ilikuwa kuvitalijimu kwa lugha ya Kiswahili, hatua ya tatu, ni kuonesha matukio muhimu katika ngano kama zilivyochunguzwa, hatua ya nne, ilikuwa ni kuchunguza namna mhusika mwanamke anavyosawiriwa na ujumbe uliofichwa na wahenga ndni ya ngano hizo. Data zilizowasilishwa katika kazi hii matikeo ya taarifa za data zilizochambuliwa. Kila swali lililoulizwa katika hojaji za mtafiti limewasilishwa kwa kujitegemea. Swali la kwanza liliuliza, jee ni kwa namna gani, ngano za Wanyankore huwasawiri wanawake? Majibu ya swali hilo yalichambuliwa kwa kuongozwa na ndharia ya ufeministi iliyojikita kufafanua mtazamo wa jamii ya Wanyankore

kuhusu wanawake.

4.3 Usawiri wa mwanamke katika ngano za jamii ya Wanyankore.

Ngano zilizokusanywa na kupembuliwa kiutafiti katika jamii ya Wanyankore, tumetambua kuwa, fasihi ya Wanyankore kupitia kijitanzu cha ngano, humsawiri mwanamke katika mtazamo hasi, jambo hilo limejidhihirisha katika baadhi ya ngano zilivyokusanywa ndani ya jamii hiyo.Katika uchanganuzi huu mtafiti alitumia jumla ya wahojiwa Hamsinina tano (45).Wakati wa utathimini mtafiti alitumia herufi (K) kuwasilisha kijiji cha Kateete, (RW) kuwasilisha kijiji Rwantsinga na (R) kuwasilisha kijiji Ruhunga.

4.4 Tathimini ya hojaji na mahojiano

